

# ESRF yaomba wananchi waichangie mawazo

**Na Mwandishi Wetu**

**Dar es Salaam**

TAASISI inayojishughulisha na Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Kijamii (ESRF), imewataka wananchi kutoa mawazo yao ili iweze kuboresha mpango wa utekelezaji wa Dira ya Taifa kuelekea mwaka 2025.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa ESRF, Dk. Bohela Lunogelo, alipokuwa akizungunza na waandishi wa habari ofisini kwake Dar es Salaam.

“Dira ya Maendeleo ya Tanzania kuelekea mwaka 2025 ilianza mwaka 2000 kwa kuweka mtazamo wa matarajio ya nchi itakavyokuwa ifikapo mwaka huo.

“Kwa kuwa mpango huu ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, tunawaomba wananchi wajitokeze kutupa mawazo yao ili tujue tufanyeje katika kufikia mafanikio zaidi, kwa sababu haya yote tunayafanya kwa masilahi ya wananchi.

- “Tunataka wananchi wambie tufanyeje ili sekta ya elimu iboreshwe, tutumie njia gani kuimarisha sekta ya afya na pia tutumie njia zipi kuimarisha masuala yote yanayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja,” alisema Dk Lunogelo.

Pamoja na maelezo hayo, baadhi ya waandishi wa habari waliohudhuria mkutano huo walitaka sekta ya elimu iimarishwe kwanza kwa kuwa bila wananchi kuwa na elimu bora, hakuna jambo la maana linaloweza kufanyika.

Kwa mujibu wa waandishi hao, elimu inayotolewa nchini haimpi uwezo Mtanzania kwa ajili ya kushindana na watu wengine katika sekta ya ajira, kwa kuwa uwezo wao wa kujieleza mdogo ukalinganishwa na nchi nyingine.